


# Madarasa bila Kuta

CHUNGUZA - GUNDUA - JIFUNZE - PENDA

## Jiunge nasi kwa ziara ya kuisisimua ya uvumbuzi katika ulimwengu wa kiajabu wa popo!

Hujambo, na karibu kwenye Madarasa bila Kuta - tukio kwako la kufurahisha katika maisha ya siri ya popo! Jina langu ni Spike na kwa kimombo mimi ni aina ya 'free tailed bat'. Ni vizuri sana kwangu kukutana na mtu anayevutiwa sana na popo. Ninatarajia kukuambia zaidi kuhusu popo, tukiwa na furaha pamoja, na kukutambulisha kwa baadhi ya marafiki zangu wa karibu zaidi!

Marafiki zetu hapa 'Bats beyond Borders' wamekuwa wakifurahia kufanya kazi nami ili kukuandalia masomo 8 ya kufurahisha. Je! ungependa kujua ni nini utakuwa unajifunza kwenye masomo?



### Hii hapa orodha ya kile kinachokuja!

somo

1

#### Popo ni nini?

Jua zaidi kuhusu popo na kinachowafanya kuwa wa kipekee sana.

somo

2

#### Tofauti ya popo

Jifunze kuhusu aina tofauti za popo, na jinsi wote ni tofauti.

somo

3

#### Popo wanaishi wapi?

Gundua wapi popo tofauti huishi (na sehemu zingine zisizo za kawaida wanazojiita nyumbani!).

somo

4

#### Popo wanakula nini?

Gundua vyakula ambavyo popo hupenda (kuna vingine unavyopenda pia?)



somo

5

## Watoto wa popo

Jua kuhusu watoto wa popo, na wanavyoitwa!

somo

6

## Vipeperushi vya ajabu

Najua ungependa kuwa na uwezo wa kupaa sio? Kupaa ni sababu nyingine kwa nini popo ni wa kufurahisha sana.

somo

7

## Vitisho kwa popo

Chunguza sababu za popo kuwa kwenye shida.

somo

8

## Unachoweza kufanya kusaidia popo!

Jua njia unazoweza kuhusika na kusaidia popo.



Katika masomo haya 8, tutakuambia mambo mengi mazuri kuhusu popo, lakini ili kukupa ladha kidogo kuhusu kitakachojiri hapa ni mambo 5 ya kufurahisha kuhusu popo:

Tunaweza kupaa!

Tunapatikana karibu kote ulimwenguni!

Baadhi yetu hutumia hila nzuri inayoitwa 'echolocation' kutafuta njia yetu (ifikirie kama picha ya sauti).

Tumekuwepo kwa muda mrefu!

Baadhi yetu tunapenda kuning'inia juu chini (kama mimi)!



## Popo na binadamu wanafanana kwa namna fulani...

"Nimekuwa nikijua zaidi kuhusu wanadamu, na nyinyi ni wa ajabu sana! Nilifurahi kusikia kwamba mnawalisha watoto wenu maziwa, hiyo ni mojawapo ya mambo yanayo tufananisha. Popo na binadamu wote ni **mamalia**."

# Popo na wanadamu wana tofauti gani? Je! unataka kujua kwa nini ninawaona wanadamu kuwa wa ajabu?



Nimesikia mambo ya ajabu sana kuhusu wanadamu. Hivi ni kweli binadamu...

... huwa macho wakati wa mchana na kulala wakati wa giza? (hiyo ni kinyume cha ninavyo kaa!)



... hawezi kupaa?!



naha!



Hapana!!

... wanatembea kwa miguu na vichwa vyao juu, badala ya kuning'inia kwa miguu yao vichwa vyao vikiwa chini?

... wanaona kwa macho yao na hawawezi kutoa mwanzi?



... anaweza kuimba na kuongea lakini anaweza tu kutoa masauti ya chini na hawezi kutoa au kusikia sauti za juu, ambazo sisi popo tunaweza kutengeneza?

Nina mengi ya kujifunza kuhusu wanadamu, lakini maisha yako yanaonekana kuwa ya kushangaza na tofauti sana na yangu!

# Kutana na baadhi ya marafiki zangu wa popo!



Wakati wa masomo yetu, baadhi ya marafiki zangu wa popo watakuja na kutusaidia. Hujambo popo wa ajabu, mngenda kujitambulisha?!



Habari, mimi ni Zeke (kwa mlio wa juu sana). Naweza kuwa mdogo sana LAKINI nina mwito wa juu zaidi wa mwito wa mwanangwi wa popo wote Kusini mwa Afrika (Karibu 210 KHz). Hiyo ni mara kumi zaidi kuliko sauti zenye mwanadamu yeyote anaweza kusikia.

Mimi ni popo mwenye masikio mafupi na kwa kimombo naitwa 'Percival's short eared trident bat'. Nilipewa jina la mwanasayansi ambaye jina lake la ukoo lilikuwa Percival, nina masikio mafupi (lakini mazuri) na nina miiba mitatu kwenye jani la pua yangu inayofanana kidogo na Uma (mkuki wenye ncha tatu).




Habari! Mimi ni Avnaya, mimi ni popo mwenye mabawa ya manjano. Najua ulifikiri popo wote walikuwa kahawia na wasiovutia. Sio mimi, mimi ni mkubwa, wa rangi ya kung'aa na mzuri!



Habari! Mimi ni Logan, mtoto mchanga wa popo aina ya 'Botswana long eared bat'. Natumia muda wangu kujilaza chini ya bawa la mama yangu (Bongi) nikinywa maziwa. Sina manyoya mengi bado lakini hiyo itakua. Nikiwa na umri wa takriban wiki nne nitaanza kujifunza kuruka na kisha nitaanza kukamata wadudu. Natumai nitakuwa nikisafiri kwa kupaa vizuri nitakapofikisha umri wa wiki sita na kisha sitahitaji maziwa tena.



Kazi Kwako!



## Shughuli ya kufurahisha kwako:

Je, unaweza kuona tofauti?

Kuna tofauti 5 kati ya picha mbili hapa chini,  
unaweza kuzipata?

